

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 6 WA WANAHISA WA BENKI

- 6.1 Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 6 wa Mwalimu Commercial Bank Plc utafanyika katika Ukumbi wa ROYAL TUGHIMBE HOTEL- Mbeya siku ya alhamisi Oktoba 6 2022 kuanzia saa 5:00 Asubuhi
- 6.2 Ajenda ni kama ifuatavyo:
  - 6.2.1 Kufungua Mkutano
  - 6.2.2 Kupitisha Ajenda
  - 6.2.3 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 5 wa Mwaka 2021
  - 6.2.4 Kujadili yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa 5 wa Mwaka 2021
  - 6.2.5 Taarifa ya Mwenyekiti
  - 6.2.6 Kupokea Ripoti ya wakurugenzi na kupitisha taarifa za hesabu za fedha za mwaka 2021
  - 6.2.7 Azimio la Gawio
  - 6.2.8 Hatua iliyofikiwa katika kuongeza mtaji wa benki
  - 6.2.9 Kupokea na kuidhinisha Malipo ya Wakurugenzi
  - 6.2.10 Kupokea na kuthibitisha Uteuzi wa Mkaguzi wa nje wa Hesabu kwa mwaka unaishia 31 Disemba 2022
  - 6.2.11 Mengineyo yatokanayo na Mkutano
  - 6.2.12 Tarehe ya Mkutano ujao
  - 6.2.13 Kufungwa kwa Mkutano
- 6.3 Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengele cha 6.2.11 hapo juu lazima atoe taarifa kwa mandishi siku tatu (3) kabla ya mkutano mkuu wa mwaka
- 6.4 Mwanahisa atakayeshindwa kuhudhuria, ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa niaba yake. Taarifa hizi zimfikie Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano. Fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya Mwalimu bank ([www.mwalimubank.co.tz](http://www.mwalimubank.co.tz)).
- 6.5 Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.
- 6.6 Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora Avenue na Mlimani Tower Dar es Salaam; katika ofisi zetu wakilishi za kanda na kwenye tovuti ya Mwalimu bank ([www.mwalimubank.co.tz](http://www.mwalimubank.co.tz)). Pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano.
- 6.7 Gharama za usafiri na malazi zitafanywa na wanahisa wenyewe.

---

Mwalimu Commercial Bank Plc

NOTISI hii imepokelewa na kuthibitisha uwepo wa akidi ya wanahisa mahususi wa mkutano huu kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Benki.

### NOTISI YA SEMINA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kuwa, kutakuwa na semina kwa wanahisa kuhusu mabadiliko ya upatikanaji wa vyeti vya wanahisa pamoja na mfumo mpya wa kielektroniki Ukumbi wa ROYAL TUGHIMBE –Mbeya Mjini siku ya Alhamisi, Oktoba 6, 2022 kuanzia saa 3:00 Asubuhi